# Athari ya Mielekeo ya Walimu wa Shule za Msingi kuhusu Ufundishaji wa Kiswahili na Mazoezi Yake katika Mtaala wa Umilisi

*Nyandwaro K. Lena*[1]*, James Ontieri*[1] *na Sangai Mohochi*[2]
[1]*Chuo Kikuu cha Rongo*
[2]*Chuo Kikuu cha Kibabii*

**Ikisiri**

**Tafiti nyingi zimeonyesha kuwa mielekeo ya walimu huwa na athari miongoni mwa wanafunzi. Sababu ni kuwa wanatangana nao kwa asilimia kubwa ya muda. Makala haya yanajadili athari ya mielekeo ya walimu kuhusu ufundishaji wa Kiswahili na mazoezi yake katika Mtaala wa Umilisi kwa kujikita kwenye Gatuzi dogo la Masaba Kusini. Mtaala wa Umilisi umechukua nafasi ya Mtaala wa 8-4-4 ambao umekuwa ukitumika nchini Kenya kwa zaidi ya miongo mitatu. Mtaala wa Umilisi kwani unasisitiza utendaji wa yale mwanafunzi amefundishwa ili kuboresha umilisi wake na kuwa na ujuzi wa kutumia maarifa aliyopata katika maisha yake ya kila siku. Makala haya yanatalii namna mielekeo ya walimu kuhusu ufundishaji wa Kiswahili imeweza kuathiri wanafunzi. Nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa ilizingatiwa katika makala haya. Data ilikusanywa miongoni mwa wasailiwa kwa kutumia mijadala ya makundi madogo ya wanafunzi kumi kutoka gredi ya kwanza hadi tatu kutoka shule kumi ambazo ziliteuliwa kimaksudi. Pia, wasailiwa waliteuliwa kimaksudi. Waliulizwa maswali na majibu yalinakiliwa na kurekodiwa na mtafiti akisaidiwa na walimu wao kwa sababu walikuwa wachanga. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa na kuwasilishwa kupitia majedwali ambayo yalijadiliwa kwa kina. Makala haya ni muhimu kwani itawasaidia walimu kujua zaidi athari waliyo nayo kwa wanafunzi na itasaidia katika kuboresha utekelezaji wa kina na ufundishaji bora wa Kiswahili katika Mtaala wa Umilisi.**

**Maneno Muhimu**: *Mielekeo, Walimu, Kiswahili, Umilisi, Athari*

**Utangulizi**

Mielekeo ni namna mtu anavyotathmini dhana au hali kwa njia chanya au hasi. Inahusu kile wanachoamini watu kuhusu matokeo ya kujihusisha na dhana, hali au kufanya kitu fulani (Ajzen na Fishbein, 2021). Tafiti mbalimbali zimeonyesha kuwa mwalimu ana athari kubwa sana anapofundisha mwanafunzi (Yadav na Baniata, 2013). Namna mwalimu anavyopanga kazi yake, na anavyowapa wanafunzi motisha huathiri matokeo ya wanafunzi moja kwa moja (Codina na wenzake, 2018).

Mielekeo ya walimu kuhusu ufundishaji wa masomo hujitokeza kupitia namna wanavyofundisha wanafunzi wao, wanavyowapa wanafunzi mazoezi, wanavyosahihisha na kuwaelekeza baada ya kusahihisha mazoezi hayo. Pia, hujitokeza kwa namna wanavyotatua na kukabiliana na tofauti za kijamii na kiuchumi miongoni mwa wanafunzi, wanavyowasaidia wanafunzi kukabiliana na changamoto wanazopitia wanapofundishwa na wanavyotangamana nao (Karabenick na Noda, 2004).

Tafiti zimeonyesha kuwa kuna uhusiano kati ya mielekeo ya walimu na motisha ya wanafunzi kutaka kujua au kusoma kuhusu lugha inayohusika. Hamer (2019) anasema kuwa mwalimu aliye na mwelekeo chanya na motisha ya kufundisha lugha huchangia mazingira chanya miongoni mwa wanafunzi anapowafundisha lugha. Liu na Zhang (2021) wanaeleza kuwa ikiwa mwalimu atakuwa na mielekeo hasi anapofundisha lugha, basi ataathiri mtazamo wa wanafunzi kwa njia hiyo hasi kwani hawatajali wala kuwa na motisha ya kufundishwa lugha inayohusika. Li na wengine (2022) wanasema kuwa walimu wanapokuwa na mtazamo chanya kuhusu lugha wanayofundisha darasani, hujenga mazingira mazuri darasani, hukuza mawasiliano yanayofaa miongoni mwa wanafunzi hasa wanapowasiliana kwa kutumia lugha inayohusika na hivyo kujenga mtazamo kubalifu miongoni mwa wanafunzi kuhusu lugha hiyo. Kwa upande mwingine, wanasema kuwa mielekeo hasi husababisha ukosefu wa mawasiliano kati ya walimu na wanafunzi wanapofundishwa lugha hiyo.

Granaos na wengine (2020) walifanya utafiti miongoni mwa wanafunzi wa chuo kikuu na kubaini kuwa walimu waliokuwa na mielekeo chanya kuhusu masomo waliyofundisha na walikuwa tayari kuwasikiliza wanafunzi walipendwa na wanafunzi. Isitoshe, wanafunzi walikuwa na ujasiri wa kuwaendea ikiwa walihitaji maelekezo zaidi kuhusu mazoezi, hali iliyoendeleza uhusiano bora kati yao. Hali hii iliathiri mtazamo wa wanafunzi kwa njia kubalifu kuhusu masomo hayo. Amalo na wengine (2022) wanasema kuwa walimu walio na mielekeo chanya kuhusu ufundishaji wa lugha hupenda kutumia mbinu bunifu na changamfu za ufundishaji ambazo zinahusisha matumizi ya teknolojia. Mbinu hizi huwachangamsha wanafunzi darasani hali inayowafanya wanafunzi kuwa na mtazamo chanya kuhusu somo hilo. Isitoshe, Li na wengine (2020) katika utafiti wao walitambua kuwa wanafunzi walioathiriwa na mtazamo chanya wa walimu na kupendezwa na namna walivyofundishwa lugha inayohusika walionyesha matokeo bora katika mitihani yao. Kwa upande mwingine, walimu ambao walionyesha mielekeo hasi walipofundisha lugha waliathiri wanafunzi kwa njia hasi hali iliyochangia matokeo duni ya wanafunzi. Liu na Jackson (2019) wanasema walimu walio na mielekeo chanya wanapofundisha lugha huwafanya wanafunzi kuwa na mshawasha wa kutaka kujifundisha lugha kwa kina, kuitumia wanapowasiliana na kufanya mazoezi ya kutosha ili kuboreha matumizi ya lugha hiyo.

Mielekeo hasi kuhusu ufundishaji wa lugha miongoni mwa walimu hujitokeza kama kutokuwa makini wanapofundisha lugha na kutokuwa na hamu ya kufundisha lugha inayohusika (Pryor na Johnson, 2018). Hali hii huwakosesha wanafunzi motisha ya kutaka kufundishwa lugha hiyo na hivyo kusababisha hali ya kutopenda lugha hiyo. Pia, Zhang na Li (2018) wanasema walimu wasiokuwa na subira kwa wanafunzi wanapofanya makosa kila wanapotumia lugha waliyowafundisha kwa njia isiyofaa na kuwarekebisha kwa ukali huwafanya wanafunzi kuwa na uoga. Hali hii huathiri mtazamo wao kuhusu lugha kwa njia hasi.

Kutokana na maelezo ya watafiti mbalimbali, ni wazi kuwa mielekeo chanya ya walimu huathiri imani na matokeo ya wanafunzi kwa njia inayofaa. Kwa upande mwingine, mielekeo hasi ya walimu huathiri mtazamo wa wanafunzi kuhusu lugha kwa njia hasi. Kulingana na Nadharia ya Kukata Tamaa (Bell, 1988), binadamu huwa na matarajio kutoka kwa wenzake. Pia, nia pamoja na majibu yao kuhusu kauli mbalimbali hujitokeza kwa matarajio hayo. Kwa hivyo, ni wazi kuwa wanafunzi hutarajia walimu wao wawe na umilisi na mielekeo iliyo kubalifu kuhusu masomo wanayoyafundisha (Takase na wenzake, 2019). Hivyo basi, ni wazi kuwa mielekeo ya walimu huathiri motisha na mielekeo ya wanafunzi kuhusu masomo wanayofundisha.

Nchini Kenya, kumekuwa na mabadiliko ya mtaala wa elimu kutoka Mtaala wa 8-4-4 hadi Mtaala wa Umilisi. Mtaala wa Umilisi ni mtaala ambao unaweka mahitaji ya mtoto mbele ya yale ya shule, mwalimu au wazazi (Abuya, 2017). Malengo yake ni kuhakikisha kuwa mtoto amehusishwa katika kujenga umilisi wake katika masomo yaliyopendekezwa na aweze kutumia umilisi wake katika mazingira yake halisi. Kiswahili na mazoezi yake ni somo ambalo ni la lazima katika Mtaala wa Umilisi. Ni somo ambalo mwanafunzi anatarajiwa kufundishwa na mwalimu kuhakikisha ana umilisi wa kutosha wa kukitumia Kiswahili katika mawasiliano yake ya kila siku na mazingira yake yote kando na darasani. Kwa hivyo pana haja ya mwalimu kuwa na mtazamo kubalifu kuhusu ufundishaji wa Kiswahili pamoja na mazoezi yake kwani tafiti zimeonyesha kuwa mitazamo yao huwa na athari ya moja kwa moja kwa wanafunzi.

Lippert (2017) anaeleza kuwa sio rahisi mwalimu mwenyewe kutathmini athari ya mielekeo yake kwa wanafunzi anapofundisha somo lake kwani kutakuwa na mapendeleo. Anapendekeza kuwa ni muhimu kutathmini athari yao miongoni mwa wanafunzi wao. Kwa hivyo makala hay yalijikita kwa wanafunzi wa gredi ya kwanza na tatu katika kubaini athari ya mielekeo ya walimu kuhusu ufundishaji wa Kiswahili na mazoezi yake. Hii ni kwa sababu mazoezi ya Kiswahili yanafanywa katika gredi ya kwanza na tatu.

**Nadharia ya Utafiti**

Makala haya yaliongozwa na Nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa iliyoasisiwa na Ajzen na Fishbein (1980). Kulingana na nadharia hii, mielekeo ya binadamu huundwa kupitia imani yake kuhusu dhana fulani. Mielekeo hutumiwa kutathmini vitendo vya watu na kulingana na nadharia hii, binadamu huchukuliwa kama kiumbe ambaye anaweza kutumia maarifa aliyopata kwa utaratibu na kufanya

uamuzi kwa sababu ni kiumbe aliye na urazini. Katika makala haya, ilichukuliwa kuwa wanafunzi wanaweza kuathiriwa na walimu kwa njia chanya au hasi kuhusu somo la Kiswahili na mazoezi yake kwa sababu wao hupata maarifa na kutangamana na walimu wao kila mara.

Isitoshe, nadharia hii inaeleza kuwa mtazamo wa mtu huathiriwa na mazingira alimo au matarajio ya wanajamii anapotenda jambo fulani. Kwa hivyo mwalimu aliye na mtazamo kubalifu kuhusu ufundishaji wa Kiswahili na mazoezi yake na anawatuza na kuwatia moyo wanafunzi wake, bila shaka wanafunzi hao watakuwa na mtazamo kubalifu kuhusu somo hilo. Nadharia hii inaeleza kuwa binadamu kutaka kufanya tendo fulani huenda moja kwa moja na tabia anayodhihirisha (Ajzen na Fisbein, 2020). Kwa hivyo utafiti huu ulitaka kubaini ikiwa walimu waliwaathiri wanafunzi walipowafundisha Kiswahili na mazoezi yake. Pia, makala haya yanabaini ikiwa nia ya wanafunzi ya kusoma Kiswahili na mazoezi yake iliathiriwa na walimu waliowafundisha. Hii ni kwa sababu nadharia hii inaeleza kuwa nia huathiri mielekeo ya binadamu kuhusu utendaji wa jambo fulani katika jamii.

**Mbinu za Utafiti**

Muundo wa utafiti ulikuwa elezi. Eneo la utafiti huu lilikuwa gatuzi dogo la Masaba Kusini lililo katika kaunti ya Kisii. Shule za msingi kumi zilichaguliwa kimaksudi. Wasailiwa walikuwa wanafunzi wa gredi ya kwanza, pili na tatu. Hii ni kwa sababu ni wao wanaofundishwa Kiswahili na mazoezi ya Kiswahili. Ikumbukwe mazoezi ya Kiswahili ni kipengele kigeni katika Mtaala wa Umilisi kwani hakikuwepo katika Mtaala wa 8-4-4. Data ilikusanywa kupitia mijadala ya vikundi lengwa iliyokuwa na wanafunzi sita hadi kumi. Wanafunzi walifafanuliwa maswali matano yaliyolenga mada ya utafiti huu, na majibu kurekodiwa na mtafiti akisaidiwa na walimu wa wasailiwa. Pia ushuhudiaji ulitumika katika kukusanya data. Mtafiti alitumia mbinu hii kutazama tabia pamoja na majibu ya kutamka kila walipoulizwa swali katika kutathmini athari ya mielekeo ya walimu kuhusu ufundishaji wa Kiswahili na mazoezi yake. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kupitia majibu ya wasailiwa na kuwasilishwa kwa majedwali huku ikitolewa maelezo.

**Matokeo ya Utafiti**

Wasailiwa waliulizwa kauli sita ambazo walijibu katika makundi sita ili kubaini athari ya mielekeo ya walimu kuhusu ufundishaji wa Kiswahili na mazoezi yake kama ifuatavyo:

**Walimu Wanavyowafundisha Kiswahili**

Wanafunzi waliulizwa ikiwa walipenda namna walimu wao walivyowafundisha somo la Kiswahili. Matokeo ya kauli hii yalikuwa kama yafuatayo:

**Gredi ya Kwanza**

**Mnapenda namna walimu wanavyofundisha Kiswahili?**

| | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| La | 2 | 20 |
| Ndio | 8 | 80 |
| Jumla | 10 | 100 |

(Chanzo: Data ya Nyanjani)

**Gredi ya Pili**

**Mnapenda namna walimu wanavyofundisha Kiswahili?**

| | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| La | 4 | 40 |
| Ndio | 6 | 60 |
| Jumla | 10 | 100 |

(Chanzo: Data ya Nyanjani)

**Gredi ya Tatu**

**Mnapenda namna walimu wanavyofundisha Kiswahili?**

| | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| La | 3 | 30 |
| Ndio | 7 | 70 |
| Jumla | 10 | 100 |

(Chanzo: Data ya Nyanjani)

Asilimia 80 ya wanafunzi wa gredi ya kwanza, asilimia 60 wa gredi ya pili na asilimia 70 ya wasailiwa kutoka gredi ya tatu walionyesha mtazamo kubalifu kuhusu kauli hii. Sababu walizotoa ni kuwa walimu wao waliwaambia ni muhimu wakipende Kiswahili kwani ni somo la lazima na muhimu katika jamii. Walisema kutokana na himizo hilo, walipenda somo la Kiswahili. Pia, walisema kuwa walimu wao waliwafundisha na kuwaelekeza kwa njia sahili na inayoeleweka hasa walipowafundisha misamiati mipya ya Kiswahili. Kutokana na majibu yao, ni wazi kuwa walimu walifundisha kwa njia inayochangamsha, hali iliyoashiria mtazamo chanya kutoka kwa walimu. Kwa hivyo, wanafunzi kuonyesha mtazamo chanya namna wanavyofundishwa Kiswahili, bila shaka ni kutokana na athari ya walimu wao. Ajzen na Fishbein (2020) wanaeleza kuwa mielekeo ya binadamu inaweza kuwa na athari kwa mielekeo ya binadamu mwingine. Hapa tunaona mtazamo kubalifu wa mwalimu ukiathiri wanafunzi. Pia, ilionyesha kuwa wanafunzi walielewa na kulipenda somo la Kiswahili kutokana na namna walimu wao walivyowafundisha kwa njia kubalifu.

Kwa upande mwingine, asilimia 20 ya wanafunzi wa gredi ya kwanza, asilimia 40 ya wanafunzi katika gredi ya pili na asilimia 30 ya wasailiwa wa gredi ya tatu, walisema hawakupenda namna walivyofundishwa Kiswahili na walimu wao. Sababu ni kuwa baadhi ya walimu wao walikuwa wakali sana walipowafundisha Kiswahili. Ikumbukwe kwamba Pryor na Johnson (2018) wanasema kuwa walimu kuwa wakali wanapofundisha somo ni ishara mojawapo ya mielekeo yao hasi kuhusu somo hilo wanalofundisha na huathiri wanafunzi kwa njia hasi. Pia, walisema kuwa baadhi ya walimu waliwafundisha vipengele vya Kiswahili kwa kutumia lugha ya kiasili, hali ambayo hawakupenda. Zaidi ya hayo, wengine walisema kuwa baadhi ya misamiati ya Kiswahili ilikuwa migumu na walipofundishwa hawakuelewa kikamilifu na walimu wao hawakuwafafanulia zaidi. Sababu mojawapo ya wao kutofafanua zaidi ni silabasi kuwa na vipengele vingi vya kufundisha kwa muda mfupi. Isitoshe, wanafunzi walisema kuwa hawakuwa na vitabu vya kusoma vya Kiswahili. Majibu yao yalionyesha kuwa tabia ya walimu kuwa wakali wanapofundisha Kiswahili iliathiri mielekeo ya wanafunzi kwa njia hasi.

### Mazoezi Wanayopewa katika Somo la Kiswahili

Mtaala wa Umilisi unasisitiza wanafunzi kufanya mazoezi ya Kiswahili ili wawe na umilisi wa kutumia lugha hii katika mazingira na miktadha halisi (K.I.C.D, 2018). Kwa hivyo, baada ya kila somo mwalimu anatarajiwa kuwapa wanafunzi mazoezi ya kufanya. Wasailiwa waliulizwa ikiwa walipenda mazoezi ambayo walimu waliwapa katika somo la Kiswahili na majibu yao yalikuwa hivi:

**Gredi ya Kwanza**

**Mnapenda mazoezi mnayopewa katika somo la Kiswahili?**

| | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| La | 7 | 70 |
| Ndio | 3 | 30 |
| Jumla | 10 | 100 |

(Chanzo: Data ya Nyanjani)

**Gredi ya Pili**

**Mnapenda mazoezi mnayopewa katika somo la Kiswahili?**

| | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| La | 6 | 60 |
| Ndio | 4 | 40 |
| Jumla | 10 | 100 |

(Chanzo: Data ya Nyanjani)

**Gredi ya Tatu**

**Mnapenda mazoezi mnayopewa katika somo la Kiswahili?**

| | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| La | 5 | 50 |
| Ndio | 5 | 50 |
| Jumla | 10 | 100 |

(Chanzo: Data ya Nyanjani)

Asilimia 30 ya wanafunzi wa gredi ya kwanza, asilimia 40 ya wanafunzi katika gredi ya pili na asilimia 50 ya wanafunzi katika gredi ya tatu walionyesha mtazamo kubalifu kuhusu kauli hii. Wasailiwa hawa walisema walipenda mazoezi ya Kiswahili ambayo walipewa na walimu wao kwa sababu yaliwasaidia kuelewa zaidi waliyofundishwa darasani. Pia, walisema yaliwasaidia kuboresha sarufi yao ya Kiswahili, hali ambayo ilijenga na kuboresha umilisi wao katika stadi nne ambazo walifundishwa katika somo la Kiswahili. Wasailiwa walisema kuwa kuna baadhi ya walimu ambao waliwaelezea na kufafanua mazoezi ambayo yalikuwa magumu kwao kwa njia ya upole. Ufafanuzi huo kwa njia ya upole ni ishara kuwa walimu walikuwa na mtazamo chanya kuhusu somo wanalofundisha (Liu na Jackson, 2019). Wasailiwa walisema kuwa mazoezi ya Kiswahili yaliwasaidia kukumbuka na kuelewa vyema waliyofundishwa darasani na mwalimu na yaliwachochea kujua mengi kuhusu somo la Kiswahili. Uchangamfu wa walimu na walimu kuwa tayari kuwapa na kuwaelekeza kufanya mazoezi ya Kiswahili uliathiri kwa njia chanya mielekeo ya wanafunzi kuhusu Kiswahili.

Kwa upande mwingine, asilimia 70 ya wanafunzi wa gredi ya kwanza, asilimia 60 ya wasailiwa katika gredi ya pili na asilimia 50 ya wanafunzi wa gredi ya tatu walisema hawakupenda mazoezi ambayo walipewa na walimu wao katika somo la Kiswahili. Walisema baadhi ya mazoezi waliyopewa yalikuwa magumu, na walishindwa kuyafanya. Walizidi kusema kuwa baadhi ya walimu hawakuwaelekeza namna ya kufanya marudio ya mazoezi ambayo walianguka, hali iliyowatamausha katika somo la Kiswahili. Liu na Jackson (2020) wanasema kuwa walimu ambao hawawasaidii wanafunzi wao kufanya marudio wala kuwapa maelekezo namna ya kufanya mazoezi huwa ni ishara mojawapo ya mwalimu kuwa na mtazamo hasi kuhusu somo hilo na bila shaka itaathiri wanafunzi wake kwa njia hasi.

Ukosefu wa vitabu, mtandao na vifaa vingine vya kufanikisha wanafunzi kufanya mazoezi kuliwafanya walimu wengine kukosa kuwapa wanafunzi mazoezi ya kufanya. Hali hii ilichangia walimu kuwa na mtazamo hasi kuhusu ufundishaji wa Kiswahili kwani walishindwa kupima umilisi wa wanafunzi kikamilifu. Sugano na Mamolo (2021) wanaeleza kuwa ukosefu wa vifaa vya kufundishia lugha huchangia katika mielekeo hasi ya wanafunzi kuhusu masomo yao, hali ambayo huathiri wanafunzi kwa njia hasi. Wanafunzi walikiri kuna ukosefu wa vitabu nyumbani (kwani wazazi walisema ni ghali) na uhaba shuleni uliwafanya kutopenda kupewa kazi ya ziada. Hali hii iliashiria kuwa mielekeo hasi ya walimu iliyochangiwa na kutopata vitabu na vifaa vingine vya kufundishia na kuwapa mazoezi iliathiri mielekeo yao kwa njia hasi.

**Kuwasiliana na Wanafunzi Wenza kupitia Lugha ya Kiswahili**

Mtaala wa Umilisi unasisitiza kuwa mwanafunzi anapaswa kutumia maarifa aliyopata katika mazingira yake halisi (K.I.C.D, 2018). Kwa hivyo, inatarajiwa kuwa mwanafunzi baada ya kufundishwa awe na uwezo wa kutumia Kiswahili katika mazingira yake halisi. Njia mojawapo ya kutumia Kiswahili katika mazingira yake ni kuwasiliana na wenzake, wazazi na jamii kwa kijumla

kupitia Kiswahili. Hali hii ya kutumia Kiswahili katika mawasiliano kwa umilisi wa juu inawezekana ikiwa mwalimu amewafundisha vilivyo, pia ikiwa mwalimu ana mtazamo chanya kuhusu Kiswahili na kuwahimiza na kuwatia moyo wanafunzi kutumia Kiswahili katika mawasiliano yao. Wasailiwa waliulizwa ikiwa walipenda kukitumia Kiswahili katika mawasiliano yao na wenzao. Matokeo yalikuwa kama yafuatavyo:

**Gredi ya Kwanza**

**Unapenda kuwasiliana na Wenzako kwa Lugha ya Kiswahili?**

| | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| La | 2 | 20 |
| Ndio | 8 | 80 |
| Jumla | 10 | 100 |

(Chanzo: Data ya Nyanjani)

**Gredi ya Pili**

**Unapenda kuwasiliana na wenzako kwa lugha ya Kiswahili?**

| | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| La | 3 | 30 |
| Ndio | 7 | 70 |
| Jumla | 10 | 100 |

(Chanzo: Data ya Nyanjani)

**Gredi ya Tatu**

**Unapenda kuwasiliana na wenzako kwa lugha ya Kiswahili?**

| | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| La | 1 | 10 |
| Ndio | 9 | 90 |
| Jumla | 10 | 100 |

(Chanzo: Data ya Nyanjani)

Matokeo ya kauli hii yalionyesha kuwa asilimia 80 ya wanafunzi wa gredi ya kwanza, asilimia 70 ya wasailiwa katika gredi ya pili, na asilimia 90 ya wanafunzi katika gredi ya tatu walisema walipenda kuwasiliana na wenzao katika lugha ya Kiswahili. Sababu walizotoa ni kuwa Kiswahili ni lugha rahisi inapotumika kama lugha ya mawasiliano ya kimazungumzo. Wengine walisema kuwa walitumia lugha ya Kiswahili kuwasiliana na wenzao kwa sababu walimu wao waliwaambia ilikuwa ni njia mojawapo ya kuboresha matamshi yao ya Kiswahili. Hapa ni wazi kuwa walimu walikuwa na athari chanya miongoni mwa wasailiwa, kauli ambayo inashadidiwa na Ajzen na Fishbein (2020) kuwa jamii huathiri mielekeo ya binadamu. Pia ni wazi kuwa wanafunzi walikuwa na nia ya kutaka kuwasiliana kupitia lugha ya Kiswahili ili waweze kuboresha mawasiliano yao. Hali hii inalandana na kauli ya Nadharia ya Vitendo Vinavyofikirika (Ajzen na Fisbein, 2020) kuwa nia huwa na athari kwa mielekeo ya wanajamii. Wanafunzi wengine walisema walimu wao waliwapa motisha na ujasiri wa kutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano yao ya kila siku. Walimu waliwaambia ni lugha ya taifa na rasmi na kwamba ina manufaa katika jamii yao.

Isitoshe, baadhi ya wasailiwa walisema walipenda kuwasiliana na wenzao kwa lugha ya Kiswahili kwa sababu ilikuwa sheria ya shule kwani kila mwanafunzi alitarajiwa kuwasiliana na wenzake kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza. Ni muhimu kutaja kuwa Nadharia ya Vitendo Vilivyofikirika (Ajzen na Fishbein, 2020) inaeleza kuwa wakati mwingine, binadamu anaweza kuwa hana nia ya kutaka kufanya kitu au akakosa kuwa na nia ya kufanya tendo hilo ila kutokana na sheria na vizingiti alivyowekewa katika mazingira yake, akajipata akifanya na kupitia kufanya jambo hilo, akawa na mtazamo kubalifu au usio kubalifu kuhusu analotenda. Ni hali ambayo wasailiwa walijipata kwayo kwani sheria ya shule ya kuwasiliana kupitia Kiswahili ilikuwa na athari chanya miongoni mwao na wakapenda kukitumia. Kwa jumla, ni wazi kuwa uchanya wa walimu kuhusu ufundishaji wa Kiswahili na mazoezi yake ulikuwa na athari chanya miongoni mwa wanafunzi wao.

Kwa upande mwingine, asilimia 20 ya wanafunzi wa gredi ya kwanza, asilimia 30 ya wanafunzi wa gredi ya pili, na asilimia 10 ya wanafunzi wa gredi ya tatu walisema hawakupenda kuwasiliana na wenzao kwa lugha ya Kiswahili. Walisema kuwa nyumbani walipenda kuwasiliana na wenzao katika lugha ya kiasili kwa sababu ya mazoea ya wazazi wao kuitumia katika mawasiliano ya kila siku. Walisema walipocheza na wenzao uwanjani, waliwasiliana kwa kutumia lugha ya kiasili wakichanganya na lugha ya Kiswahili. Walisema kuna baadhi ya walimu ambao hawakuwa makini ikiwa wanatumia Kiswahili au lugha ya kiasili. Kwa hivyo hali hii ya walimu kutokuwa makini iliwafanya kupuuza kutumia Kiswahili wanapowasiliana na wenzao. Matokeo haya yalionyesha kuwa wakati mwingine, binadamu anaweza kuunda mtazamo wake bila kuathiriwa na binadamu mwingine.

**Kueleza, Kuelewa na Kutatua Masuala Ibuka kwa Lugha ya Kiswahili**

Ni muhimu kutaja kuwa Mtaala wa Umilisi unasisitiza wanafunzi wafundishwe masuala ibuka katika masomo yote Kiswahili kikiwemo ili wawe na umilisi na ujuzi wa kukabiliana na masuala hayo katika maisha yao ya kila siku. Taasisi ya elimu ya Kenya (2006) inaeleza kuwa masuala ibuka ni mambo ambayo yamekuwepo na huathiri jamii kwa kiwango kikubwa. Simala (2016) anasema kuwa ni mambo ambayo mara nyingi hayatambuliki katika jamii lakini huwa na athari chanya au hasi katika maisha ya binadamu. Kwa hivyo ni muhimu wanafunzi wafundishwe na kuelimishwa jinsi ya kukabilinana na hali hizo ili wawe na maisha bora na uhusiano unaofaa na wanajamii wengine. Katika utafiti huu, wasailiwa waliulizwa ikiwa walipenda namna walimu wao walivyowafundisha masuala ibuka katika somo la Kiswahili. Kupitia usaidizi wa walimu wao, wasailiwa walielezewa maana ya masuala ibuka kupitia mifano mbalimbali katika somo la Kiswahili. Wasailiwa walielewa na kukiri kufundishwa masuala ibuka katika somo la Kiswahili na kufanya mazoezi yanayohusisha masuala ibuka. Matokeo yalikuwa kama yafuatavyo:

**Gredi ya Kwanza**

**Mnaweza kutatua masuala ibuka katika lugha ya Kiswahili?**

| | **Umaratokezi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| La | 1 | 10 |
| Ndio | 9 | 9 |
| Jumla | 10 | 100 |

(Chanzo: Data ya Nyanjani)

**Gredi ya Pili**

**Mnaweza kutatua masuala ibuka katika lugha ya Kiswahili?**

| | **Umaratokezi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| La | 2 | 20 |
| Ndio | 8 | 80 |
| Jumla | 10 | 100 |

(Chanzo: Data ya Nyanjani)

**Gredi ya Tatu**

**Mnaweza kutatua masuala ibuka katika lugha ya Kiswahili?**

| | **Umaratokezi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| La | 1 | 10 |
| Ndio | 9 | 90 |
| Jumla | 10 | 100 |

(Chanzo: Data ya Nyanjani)

Kulingana na kauli hii, asilimia 90 ya wasailiwa katika gredi ya kwanza, asilimia 80 ya wasailiwa katika gredi ya pili, na asilimia 90 ya wasailiwa katika gredi ya tatu, walisema walikuwa na uwezo wa kuelewa, kueleza na kutatua masuala ibuka katika lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia walivyofundishwa na kuelekezwa na walimu wao. Walisema walimu wao waliwaeleza kuhusu masuala hayo kwa njia sahili huku wakitumia mifano sahili kutoka katika mazingira yao. Pia,

wanafunzi walisema walimu waliwafundisha kupitia vibonzo na picha mbalimbali kutoka kwenye mtandao, hali iliyofanya ufundishaji kuwa bora, bunifu na wa kufana. Ni muhimu kutaja kuwa Walsh na wenzake (2020) wanaeleza kwamba mwalimu aliye na mtazamo kubalifu kuhusu somo analofundisha, hujaribu kupanga somo lake kwa njia inayoeleweka, hutumia mbinu za ufundishaji bunifu na sahili hali ambayo huwaathiri wanafunzi kwa njia chanya. Hali hii ilijitokeza katika utafiti huu kwani uelewa na kujaribu kutatua masuala ibuka kwa kutumia lugha ya Kiswahili kulionyesha mtazamo chanya miongoni mwa wanafunzi.

Waliokuwa na mtazamo hasi kuhusu kauli hii walikuwa asilimia 10 ya wanafunzi katika gredi ya kwanza, asilimia 20 ya wanafunzi katika gredi ya pili na asilimia 10 ya wanafunzi katika gredi ya tatu. Walisema hawakuelewa, wala kutatua masuala ibuka kupitia lugha ya Kiswahili. Walisema walimu wao waliwaeleza na kuwaelekeza kupitia lugha ya kiasili huku wakichanganya Kiingereza na Kiswahili. Pia, walisema kuwa walimu wao waliwafundisha kwa Kiingereza masuala ibuka mengi hasa yanayohusiana na afya ya miili yao katika somo la sayansi. Ingawa asilimia ndogo ya wasailiwa walionyesha mtazamo hasi kuhusu kauli hii, walimu wao kuchanganya lugha walipowafundisha kuliwaathiri kwa njia hasi.

**Mawasiliano na Walimu kwa Lugha ya Kiswahili**

Mtaala wa Umilisi unahimiza matumizi ya maarifa yapatikanayo katika mazingira halisi ya mwanafunzi. Mazingira mojawapo ni kuwasiliana na wenzake, wazazi na walimu. Wasailiwa waliulizwa ikiwa walipenda kuwasiliana na walimu wao kupitia lugha ya Kiswahili na matokeo yalikuwa kama yafuatayo:

**Gredi ya Kwanza**

**Unapenda kuwasiliana na walimu kwa lugha ya Kiswahili?**

| | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| La | 3 | 30 |
| Ndio | 7 | 70 |
| Jumla | 10 | 100 |

(Chanzo: Data ya Nyanjani)

**Gredi ya Pili**

**Unapenda kuwasiliana na walimu kwa lugha ya Kiswahili?**

| | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| La | 3 | 30 |
| Ndio | 7 | 70 |
| Jumla | 10 | 100 |

(Chanzo: Data ya Nyanjani)

**Gredi ya Tatu**

**Unapenda kuwasiliana na walimu kwa lugha ya Kiswahili?**

| | Umaratokezi | Asilimia |
|---|---|---|
| La | 1 | 10 |
| Ndio | 9 | 90 |
| Jumla | 10 | 100 |

(Chanzo: Data ya Nyanjani)

Asilimia 70 ya wanafunzi katika gredi ya kwanza, asilimia 70 katika gredi ya pili na asilimia 90 ya wanafunzi katika gredi ya tatu, walisema walipenda kuwasiliana na walimu wao katika lugha ya Kiswahili. Walimu walikuwa tayari kila mara kuwasiliana nao kwa Kiswahili. Hali hii iliwafanya wasailiwa kuwa na uzoefu wa kuwasiliana na walimu wao kwa Kiswahili. Pia, walisema walimu waliwatia moyo kuwa kupitia uzoefu wao wa kuwasiliana nao kwa Kiswahili, wangeweza kuboresha msamiati wao na kujua mambo zaidi. Kila walipotumia Kiswahili kwa usahihi walipowasiliana na walimu wao, walituzwa kwa kupigiwa makofi, kutuzwa zawadi kama penseli, na kupongezwa kwa

maneno chanya kama vizuri sana, hongera na mengine mengi tu. Ni muhimu kutaja kuwa wakati mwingine binadamu anaweza kuwa hana nia ya kufanya jambo fulani lakini akalazimishwa kufanya tendo hilo na kupitia uzoefu wa kulifanya akaunda mtazamo chanya au hasi kuhusu hali hiyo (Ajzen na Fishbein, 2020). Hali hii ilijitokeza pale ambapo wasailiwa walisema kulikuwa na sheria shuleni iliyowaelekeza kuwa wanapaswa kuwasiliana na walimu wao kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza. Kwa hivyo, uzoefu wa kutumia Kiswahili katika mawasiliano yao na walimu wao kuliwafanya wakawa na mielekeo chanya kuhusu kauli hii. Kutokana na motisha, sheria na ushauri kutoka kwa walimu wao, ni wazi kuwa waliathiriwa kwa njia chanya na walimu wao na hivyo wakawa na mtazamo chanya wa kutumia Kiswahili katika mawasiliano yao na walimu.

Kwa upande mwingine, asilimia 30 ya wasailiwa katika gredi ya kwanza, asilimia 30 katika gredi ya pili na asilimia 10 katika gredi ya tatu, walisema hawapendi kuwasiliana na walimu wao kwa lugha ya Kiswahili. Walisema kuwa baadhi ya walimu waliwasiliana nao kupitia mchanganyiko wa Kiswahili na lugha ya kiasili. Ni hali ambayo mtafiti kupitia ushuhudiaji aliiona hasa katika shule za serikali hususani miongoni mwa wanafunzi wa gredi ya kwanza na ya pili na walimu wao. Katika shule za kibinafsi, walimu waliwasiliana na wanafunzi wao kupitia mchanganyiko wa lugha ya Kiingereza na Kiswahili ila msisitizo uliwekwa sana katika matumizi ya lugha ya Kiingereza. Wanafunzi hawa walisema kuwa walipenda kuwasiliana na walimu wao katika lugha ya Kiingereza kwa sababu walimu wao pamoja na wazazi wao waliwasisitizia umuhimu wa kujua na kuzungumza lugha ya Kiingereza. Pia walisema walituzwa kila walipoonyesha uwezo wa kutumia Kiingereza katika mawasiliano yao, hali iliyowapa motisha ya kutumia Kiingereza. Walisema kuwa hata walimu wao wa Kiswahili walitumia Kiswahili walipowafundisha darasani tu, lakini katika miktadha mingine, walitumia Kiingereza. Hali hii iliashiria kuwa walimu waliofundisha shule za kibinafsi waliweka msisitizo kuwa mawasiliano yawe kwa lugha ya Kiingereza na hivyo ikawa na athari kwa wanafunzi katika matumizi ya Kiswahili katika mawasiliano. Miongoni mwa baadhi ya walimu wa shule za serikali hawakutilia maanani lugha ya mawasiliano, na hali hii ikawa na athari miongoni mwa wanafunzi wao.

## Hitimisho

Kupitia matokeo yaliyoonyeshwa na wanafunzi katika utafiti huu, ni wazi kuwa asilimia kubwa ya mielekeo yao kuhusu somo la Kiswahili na mazoezi yake imeathiriwa na walimu wao. Hali hii inaonyesha kuwa mazingira huathiri pakubwa mtazamo wa mtu kuhusu hali, dhana au kauli fulani. Kwa hivyo, pana haja ya walimu kujaribu kuwa na mielekeo chanya kuhusu ufundishaji wa Kiswahili ili kuathiri wanafunzi kwa njia chanya, hali ambayo itasaidia utekelezaji wa Mtaala wa Umilisi kikamilifu hasa katika ufundishaji wa Kiswahili. Hali hii itawezekana ikiwa walimu watabuni njia bunifu ya kufundisha Kiswahili na mazoezi yake na kuwa wachangamfu na tayari kuwasaidia wanafunzi kwa njia bunifu.

## Marejeleo


Ajzen, I., na Fishbein, M. (2020). *Understanding Attitudes and Predicting Social Behaviour*. Eaglewood Cliffs, NJ: Prentice-Hall.

Codina, N., Valenzuela, R., Pestana, J. V., na Gonzalez-Conde, J. (2018). Relations between Student Procrastination and Teaching Styles: Autonomy, Supportive and Controlling. *Psychology*. *9*, 809. doi: 10.3389/fpsyg.2018.00809.

Fraser, L. E. (2014). Teacher Efficacy Beliefs: How General Teachers Feel towards English Language Learners. *Capstones paper 828*. Uk. 1-56.

Granaos, F. C. na wenzake. (2020). A Descriptive Study on the Training and Attitude of Future Teachers towards Educational Inclusion. *Sustainability, 12*(19), 1-14.

Hamer, L. na Keefe, R. (2013). Achieving Change in Students' Attitude towards Group Projects by Teaching Group Skills. *Journal of Higher Education Theory and Practice,* 25-33. https://via.library.depaul.edu/buspubs/71.

Karabenick, S. A. na Noda, P. A. C. (2004). Professional Development Implications of Teachers' Beliefs and Attitudes toward English Language Learners. *Biling. Res. J., 28*(1), 55-75.

Liu, L. na Jackson, J. (2019). Building Learner Self Belief in Oral Communique via Remarks. *Journal of Language Teaching and Research, 10*(3), 647-660.

Pryor, N. J. na Johnson, C. C. (2018). Assessing the Impact of Instructors' Terrible Mindset on Pupil Fulfilment. *Teachers College Record, 120*(10), 1-40.

Simala, I. K. (2016). Fasihi Ibuka ya Kiswahili. Hli na Mustakabali Wake. Katika Mwita, L. C. (Mh.), *Kiswahili na Utandaazi* (116-136). Nairobi: Twaweza Comunications.

Sugano, S. G. C. na Mamolo, L. A. (2021). The Effects of Teaching Methodologies on Students' Attitude and Motivation. *Meta-analysis. Int. J. Instr, 14*, 827–846. doi: 10.29333/iji.2021.14348a.

Taasisi ya Elimu ya Kenya (2006). *Kiswahili Sekodari: Mwongozo wa Mwalimu*. Nairobi: Taasisi ya Elimu.

Takase, M., Niitani, M., Imai, T. na Okada, M. (2019). Students' Perceptions of Teaching Factors that Demotivate their Learning in Lectures and Laboratory-Based Skills Practice. *Int. J. Nurs. Sci.*, *6*, 414–420. doi: 10.1016/j.ijnss.2019.08.001.

Ulug, M., Odzen, S. M. na Eryilmaz, A. (2011). The Effects of Teachers' Attitudes on Students' Personality and Performance. *Proc. Soc. Behav. Sci., 30*, 738-742.

Walsh, P., Owen, P. A. Mustafa, N. na Beech, R. (2020). Learning and Teaching Approaches Promoting Resilience in Student Nurses: An Integrated Review of the Literature. *Nurse Educational. Practicet*, *45*, 8. doi: 10.1016/j.nepr.2020.102748.

Yadav, M., na Baniata, H. (2013). Factorizing Demotivation, Findingmotivation: A Constructive Approach to Quality Enhancement. *Procedia Soc. Behav. Sci.*, *70*,120–130. doi: 10.1016/j.sbspro.2013.01.047.

Zang, Y. na Li, Y. (2018). The Impact of Instructors' Negative Attitude Closer to Secomd Language Errors on College Students' Anxiety aad Willingness to Communicate in English. *Journal of Teaching and Research, 9*(5), 948-956.